

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA HALMASHAURI YA JIJI



Kumb. Na. MCC.C.40/44/11/152

Tarehe 20.06.2024

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza anapenda kuwatangazia wakazi wa Mwanza wenyе sifa, nafasi 96 za ajira ya muda ya kukusanya mapato (Revenue Collectors) katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

KAZI NA MAJUKUMU

1. Kukusanya mapato mbalimbali ya Halmashauri.
2. Kutunza kifaa cha kukusanya Mapato (POS).
3. Kuhakikisha fedha zote zinazokusanywa zinapelekwa Benki kila siku.
4. Kuhakikisha makusanyo yote yanafanyika kwa kutumia POS mashine.

SIFA ZA MWOMBADI

- i. Awe Raia wa Tanzania na mwenye utambulisho wa Taifa (NIDA)
- ii. Awe ni mhitimu wa angalau kidato cha Nne mwenye ufaulu wa Daraja la Nne na Kuendelea.
- iii. Awe na wadhamini 2 wenyе makazi ya kudumu katika Wilaya ya Nyamagana, na wanaomiliki mali zisiyohamishika.
- iv. Awe mwadilifu na ambaye hajawahi kupatikana na hatia Mahakamani.
- v. Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kujituma pasipo kusimamiwa.
- vi. Awe tayari kufanya kazi katika Kata yoyote ya Halmashauri kwa kipindi kisichopungua mwaka Mmoja.
- vii. Awe na uzoefu wa kukusanya Mapato na mwenye historia nzuri ya uaminifu
- viii. Awe na umri kati ya miaka 18 hadi 35.
- ix. Menye ujuzi wa kuendesha Pikipiki watapewa kipaumbele.

MAMBO YA JUMLA YA KUZINGATIA

- i. Waombaji waambatishe vivuli vya vyeti ya Elimu, maelezo binafsi (CV) na nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- ii. Aidha, barua zibandikwe picha Mbili (2) za passport size za hivi karibuni.
- iii. Katika barua ya maombi, weka namba ya simu inayopatikana muda wote.
- iv. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 03.07.2024 saa 9:30 Alasili.
- v. Maombi yote yaelekezwe kwenye Anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi,

Halmashauri ya Jiji,

S.L.P 1333,

MWANZA.

Imetolewa na:

WAKILI; KIOMONI KIBURWA KIBAMBA
**MKURUGENZI WA JIJI
MWANZA.**

**MKURUGENZI WA JIJI MWANZA
MWANZA**